John Wandunga: Asante Commission. Jina langu ni John Lumbasi Wandunga kutoka Kimanget East Kabras location. Yangu ni kusema ya kwamba, tangu tuwe katika ukoloni na hata tupate uhuru serikali za mitaa zilikuwa zimenunua ploti na watu wanajenga manyumba ya biashara na ikawa kila mwaka huyu mtu analipa rent kwa ploti hiyo. Na hata wakati huu wangali wanalipa hata ikiwa umejenga gorofa hauna uhuru kwa hiyo ploti. Kwa hivyo ningependa katiba ya sasa ifikirie hapo ikiwa mtu alijenga nyumba kwa ploti ya county council na amelipa miaka na miaka, atakuwa squatter miaka mingapi? Katiba ya sasa napendekeza ya kwamba huyu mtu apewe title deed, awe akimiliki hiyo ploti ambayo alipewa na county council.

Ya pili, katika Kenya tumekuwa na watu wengi ambao hawajiwezi na upande wa elimu tunataka watoto wapate elimu. Ningependelea kwamba katiba ya sasa ikiwezekana watoto wapate masomo ya bure kutoka darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Kwa sababu kuna watu wengi ambao hawajiwezi, kuna watu wengi ambao wamekufa na wamewachwa mayatima au mayatima wamewachwa kama wako wadogo hawawezi kujiweza, kwa hivyo elimu ikiwa ya bure hawa watoto watapata masomo na watapata akili ambayo wanaweza kuishi maisha yao katika nchi hii.

Na nikimalizia, upande wa utawala ningependa chief na assistant chief wawe wakichaguliwa moja kwa moja na wananchi ambao wamejua fulani anaweza kutusaidia kwa njia hizi, kwa sababu hao ndio msingi wa maendeleo katika nchi yetu ya Kenya.

Na vile tunachaguliwa kutoka Nairobi tunaletewa mtu ambaye hata hajapeleka mtoto kwa nursery amekuwa mtawala. Kwa hivyo katiba ikipenda hao watawala wachaguliwe moja kwa moja kutoka kwa wananchi. Asanteni kunisikiliza.

Com. Abida Ali: Kuja ujiandikishe Yohana Mukhanya.

Yohana Mukhanya: Ni asante sana Commissioners, mimi ni Yohana Mukhanya nawakilisha Kanisa la Marafiki. Kwanza ningependa kwamba mamlaka ya rais yapinguzwe na wabuni cheo cha waziri mkuu. Mahakama iwe huru, isiingiliwe na mkubwa yeyote, sheria ikishapitshwa imepitishwa na mtu ahukumiwe kisheria.

Makanisa yawe huru kuikosoa serikali ikiwa kuna lazima, maana huwa tunawekewa vizuizi kwamba makanisa yasiingilie siasa na sisi sote ni wananchi.

Vyema vimekuwa vingi vya kisiasa, afadhali viwe vitatu au vinne maana umekuwa tu ni uwanja wa fujo hatuelewi tunafanya nini. Nafikiri mambo yangu yamefikia hapo, asanteni.

Com. Abida Ali: Asante, jiandikishe. Jafred Mutoso, Eliud Muyeko.

Eliud Muyekha: Thank you Commissioners, I am known as David Muyekha a voter in Malava. I have the following contributions to make. I first want to begin by saying that of late there is Aids which is threatening people's lives. So I suggest that a compulsory Aids test for all Kenyans should be carried out so that those who test HIV positive are stamped at a place where at least somebody who develops this(?) in another can see to curb the increase of such infection.

In addition to that I also want to make the following contribution, that police brutality should be stopped. In Kenya we have a lot of police brutality, police harassment is very common they shoot very innocent people just on mere suspicion. We know that life is precious; it cannot be bought using any given amount of money, talk of even trillions.

In addition to that, I want to stress that policemen are not given adequate training. Policemen perform a very important role, you know they are the people who keep and maintain law, and so they should be well versed, well furnished with the law of the land. So I suggest that they should be given a two-year training course.

In addition, I also want to talk about the institution of the president. I am doing that because this is a very sensitive area. Of late people are engaged in a lot of argument about who should take over the presidency of this country. So I want to say that the president of Kenya should be a Christian who is God fearing and a sober-minded person who doesn't strictly drink. We should not allow desperate alcoholic psychopaths to head us.

The President should be a person who has never committed any offence and should produce a certificate of good conduct. He should not necessarily have served as an MP, even a person who is outside the parliament should be given the opportunity to vie for that post. Also he should declare his wealth and in any case should be immensely wealthy to avoid corruption. The post

of the president should not be confined to specific communities. We know that in Kenya we have forty two communities so all these 42 communities should be represented equally, which is a problem that most countries have faced. To say just but a few examples, we have our neighbors Rwanda here and Burundi, so we need equal representation. So in that case I want to say that the country should be divided into parts so that each part is given the opportunity to produce a president.

Interjection Com. Abida Ali: Please summarize now.

Eliud Muyekha: Okey, I also want to say that I had quite a lot but because of time I shall beg for some little time to finish up..

Interjection Com. Abida Ali: We shall read your document, so highlight what you think is important and hand in your document.

Eliud Muyekha: Okey so let me wind up. The president should be restricted to one post only. The president's and MPs' salary should be taxed. Gender equality should be exercised so that female are given a chance to rule. The President's tribe should not hold key positions in the Government to avoid tribal(?).

Com. Abida Ali: Thank you very much, we will read your document you shouldn't worry. Thank you. Mageso Mathias, David Yavusumba.

David Yavusumba: Honorable Commissioners. I am David Yavusumba from Kabras sub location. I have a number of things to put across. I want to say that the brewing of chang'aa should be legalized as long as the brewers obtain a trade license from the authority. This is because chang'aa has been known to fetch massive wealth to the brewers, and to the fact that it creates employment opportunities.

I want also to say that military education should be compulsory for all able-bodied in Kenya to enable them contain and withstand difficult situations especially during times of wars.

Also I wish today that there should be a special commission to regulate salaries of members of parliament to prevent unscrupulous Members of Parliament from increasing their salaries and as a result impoverishing taxpayers.

Also I want to talk about the land tenure system that the individual owner operator should be abolished and be replaced by the state-owned land tenure system to enable landless people to carry out farming activities. This will enable us avoid a situation where one person is owning 200 acres of land and another person is owning zero, and that person does not use the land.

Finally, I would wish to suggest that in future, Kenyans should be adequately prepared when such an exercise takes place. In

the first place I don't know what the constitution contains. I would wish to suggest that, the word constitution should be introduced as a subject in secondary school so that by the end of the four year course a student having gone through the four year course is able to know what the Constitution is so that if told to change can change the Constitution. I think this time we are not ripe enough to change the constitution because we don't know what it is, or else the government should print pamphlets and booklets and distribute to all Kenyans so that we are able to obtain information concerning the Constitution. Otherwise thank you very much for paying me all these.

Com. Abida Ali: Please register. Samuel Musosi, Johnson Wamache, Tunde Izakiah, Sakwa Wambulwa.

Sakwa Wambulwa: Tume ya marekebisho, wananchi wa Malava kwa majina mimi naitwa Sakwa Mbulua Mkaswa Mkai. Kwa upande wangu nataka kuchangia marekebisho ya katiba kwa upande, ukija kwa upande wa inquiry Commission. Kwa upande wa inquiry commission mimi naonelea kwamba iwapo mustel fulani umetokea kwa nchi pengine tunataka kuchunguza ni president mwenye amekosa makosa, inatakikana Parliament committee iwe ndio inadhinisha inquiry commission sio rais kwa sababu ikifikia mahali fulani inaonekana inaenda upande mwingine, hiyo commission inazimia bila kujua yale malengo yenye ilikuwa inatakikana yafikiwe kabla haijafikiwa.

Kwa upande wa elimu, mimi naona education system inatakikana iendelee na Review kwa sababu ikifanyiwa review kila wakati it will be coping up with the standard of the times.

Kwa upande wa madaktari, mimi naona ya kwamba daktari wakati anapoendelea na masomo yake, nafikiria ya kwamba anapitia wakati mwingi kuangalia jinsi inavyotakikana aangalie maisha ya binadamu, kwa hivyo mimi naona ya kwamba madaktari inatakikana wawe na committee yao ya kuangalia jinsi mishahara yao inatakikana ipangwe.

Nikikuja kwa aid programmes yaani yale mambo yenye inatoka ng'ambo kwa donors. Inatakikana kamati iundwe ya kuangalia jinsi huo msaada ulivyokuja uende mpaka mahali ulitakikana ili ihakikishe kwamba ule msaada umefanya kazi yenye ilipangiwa ifanye. Yaani tuwe na monitoring na evaluation committee ya kuangalia jinsi hiyo misaada imefanya kazi.

Kwa upande wa land adjudication: kwa upande wa land tunaonelea kwamba tangu uhuru mababa zetu ama mababu zetu wengine walifanikiwa kupata land title deeds lakini wengine hawakufanikiwa. Kwa hivyo tunaona ya kwamba serikali iangalie ni muda gani haya mashamba yaligawiwa watu, iwapo watu hao hawajiwezi basi serikali itusaidie kupata title deed bure bila kulipa chochote. Serikali iangalie iwapo mtu ni maskini na tangu apewe hilo shamba na land title deed ingali kwa board, wahakikishe kwamba hilo shamba angalau mwenyewe amepata land title deed ili kama ni wakati wa kupata kitu kama loan iwe security ya kwenda kwa co-operative ndio apewe mkopo afanyie kazi.

Kwa upande wa local industry, naona ya kwamba to protect the local industry tunaona ya kwamba bidhaa zenye zinaundwa

hapa nchini kwa mfano sukari, hatuna haja ya kuingiza sukari hapa kwa maana tuna bidhaa kama hizo. Kwa sababu kuleta bidhaa kama hizo hapa inaleta matatizo kwa wakulima kwa mfano hapa Malava mambo hayo yanafanya miwa yao inapunguzwa hadi kiwango cha chini sana kulipiwa.

Com. Abida Ali: Tutasoma mengine. Moses Kono.

Moses Kono: Mimi naitwa Moses Kono kutoka Makunga sub location Kabras, nina maoni machache ya kupeana wakati wa leo. Kwanza naonege kuhusu president, president asiwe mtu ambaye ako kwa chama fulani. Achaguliwe bila kupitia kwa chama ili ahudumie vyama vingine vyote, asibague chama akiwa president.

Kuhusu retirement, mtu akiretire huwa anaenda nyumbani na sioni kwa sababu ya kupea president nyumba na ofisi. Asiwe na ofisi, yeye labda apewe tu marupurupu kidogo na aende nyumbani kwake apumzike. Kwa sababu tukiwa na kita mtu apate ofisi apate manyumba tutakuwa na president kumi kuna manyumba kumi na ofisi kumi haina maana.

Kuhusu watoto, napendekeza ya kwamba kila mtoto azaliwaye ajulikane mzazi wake ili watoto wa kurandaranda mtaani wasipatikane. Mtoto akizaliwa lazima watu wa hospitali waulize mama ama msichana baba ya mtoto huyo ili ajulikane kabisa apatiwe mzazi wake.

Mambo huhusu mashamba, shamba liwe na mtu mmoja ambaye ni mzee, akigawanya hilo shamba kwa watoto wake asimpe cheti cha kurithi ili mambo ya uuzaji na ununuzi wa mashamba ipungue. Kwa sababu ukimpa mtoto shamba akitaka kuuza huna ruhusa tena. Kuhusu anaponunua shamba ni lazima wazee wa mtaa ama wazee wa jamii wajue ni kwa nini mtu anauza shamba na anauza kwa nani.

Mambo kuhusu kifo, katika mila zetu ni wavulana ambao wanapewa shamba na msichana huwa ameolewa hawezi kutoka kwake tena arudi nyumbani apewe shamba lingine. Ni watoto wavulana watapewa shamba. Na msichana kama anarudi nyumba atakaa na wazazi wake bila kupewa shamba, kwa sababu akipewa shamba ataliuza tupate mtu mwingine kwa boma.

Nahimiza kwamba mila ya kila watu iheshimiwe. Mtu asiamke tu asubuhi na kusema ya kwamba neno fulani litolewe. Kama ni mila ya Waluhya wakisema wavulana watahiriwe, watahiriwe, ni mila yao. Ikiwa wamesema wasichana watahiriwe iende hivyo hivyo vile wenyewe walichagua. Kwa sababu nikisema ya kwamba mtu atasema tu kesho mila fulani itolewe basi itakuwa mwingine akiwa mtawala atatulazimisha mila yake ambayo si yetu. So mila ya kila watu iheshimiwe.

MP na councilors waende safari mbili peke yake. Na MP ama Councillor ambaye hawahudumii watu wake arudi nyumbani.

Interjection Com. Abida Ali: La mwisho.

Moses Kono: Ya mwisho, hiyo ndio ilikuwa ya mwisho, wajumbe hao na macouncillor wakifanya makosa arudi nyumbani kwa watu wake tena achuguliwe upya.

Com. Abida Ali: Asante, jiandikishe tafadhali. Isiah Chekuani, Henry Ndombi.

Henry Ndombi: Commissioners kwa majina ni Henry Ndombi natoka Maira sub location Kabras. Yangu la kwanza ningependekeza ya kuwa president wetu asiwe mtu wa kuchagua permanent secretaries, parastatal heads na ambassadors, hiyo ipitiswe na bunge.

Watu kama PCs, DCs na Deputy Secretaries wawe watu wa kuchaguliwa na Public Service Commission. Chiefs to be regarded as traditional leaders, hao watu washugulike sana na mambo ya utamaduni wa kunyumbani na wao wachaguliwe baada ya miaka mitano na wananchi.

Jambo la nne ni ya kwamba(?) serikali yetu iweke muda kwa korti, mtu akishtakiwa ajue ya kwamba atakuwa ndani au hayo makosa yake yatashughulikiwa kwa muda fulani kwa sababu tukiwa na cases kama za mashamba huchukua hata miaka minne au miaka mitano.

Jambo la pili, recruitment: hii idara ya polisi, health, ualimu na army, tuko na corruption nyingi sana. Ningependekeza ya kuwa wasiwe wakiangalia mambo ya ukabila. Mtu achaguliwe kulingana na maumbile yake na elimu yake wasiangalie kwa mambo ya ukabila. Ni hayo tu ninayo. Mungu awabariki.

Com. Abida Ali: Jiandikishe tafadhali. Memeti Momasi.

Wellington Memet: Macommissioners, kwa majina ni Wellington Memet Mumasi. Na ningependa kufanya tu summary maanake mengi yamesemwa. Kwanza napendekeza kwa Constitution Review ya kwamba katiba ibadiliswe ili wanafunzi wote kutoka kiwango cha elimu ya msingi mpaka University wakati wa kufanya budget, budget iwe ikifanywa ili wanafunzi wote wapate haki, pesa ziwe. There should be a vote for that allocated to cater for that.

Pili, courts zetu ziwe na prosecutors wawe wale watu wenye wamefanya legal law, wale wanasimamia mambo ya prosecution, maanake watu wengi kama case ikienda huko wale ma- prosecutor ambao tuko nao wananchi hunyanyaswa zaidi.

Kuna watu wengi wanaumia kulingana na kutopata matibabu. Kila mwananchi tena vote iweko akienda kwa matibabu serikali iwe inaweka vote ya pesa ya kugharamia matibabu kwa wananchi mpaka wakati huu wote wanalipa taxation. Kwa hayo machache maanake ningekuwa na mengi lakini yote yamesemwa na sitaki kurudia tena. Kwa hayo machache Commissioners

asante kwa kunisikiza.

Com.Abida Ali: Asante Mzee. Sophia Mercy, Mashati Mukavana, David Ochanu.

David Ochanu: The Commissioners, my fellow Kenyans my names are David Ochanu. One, it has been said severally that ignorance of the law has got no defense. I tend to propose that it should have defense because most of these laws that are governing us have not gotten access to the citizens. One buys a stolen item for example and then goes to sell it at a public market, somebody comes and buys it honestly out of his own sweat halafu anashikwa na hiyo kuku. Yeye inaonekana kwamba kifungo chake ama punishment yake ni kubwa sana hata kuliko yule ambaye aliiba na yeye alinunua kuku huyo kwa kutojua kwamba ni ya wizi. Because of that, I wish to propose that the government should look at that and see how much civic education about this constitution that we are talking about can reach the citizens. Because even right now I am not in a position to have evaluated the old constitution to know the areas that are supposed to be amended or not.

The police professional ethics is appalling, I am suggesting that the training to be looked into very much. The current one is harassment oriented. Unakosana na mtu kwa mpaka kule nyumbani na kwa sababu huyo mtu ana pesa, anaenda ananunua police wanakuja kushika wewe. The same person takes an advocate and files a case very far away from your area of residence. I want to propose that cases to be filed in the nearest courts available so that we should not punish unfairly. Also under the same police professional ethics, we have had very unfair arrests beside on individual differences. You reach the cells umewekewa bangi, unawekewa chang'aa ambayo hata haukuwa nayo. Thank you very much, there is a last one.

The government poverty eradication programme has been a failure and because of that the gap between the richest and the poorest has continued to widen and this has created a loophole whereby those seeking elective posts are using handouts to bribe these poor Kenyans so that they get the votes and this has made us realize poor representation in parliament and civic bodies. Over the same I want also to propose in order to safeguard our economy that is ailing, the government should look into the issue of buying vehicles that are easy to maintain for government civil servants and so on. Because we have realized very expensive cars being bought and I think this is uneconomical to this country. Thank you.

Com. Abida Ali: Thank you please register. Wechuli Francis.

Francis Wechili: Wageni wetu the Commissioners, majina ni Wechulo Francis. Langu la kwanza nitaangalia katika kazi ya leo ama shughuli ya leo tukijaribu kusahihisha makosa mahali fulani ama kuunda kitu fulani ili kisaidie wananchi wa Kenya.

Na kitu cha kwanza huwezi kuwa mwananchi wa Kenya kama uko landless, sielewi katiba itasaidia nani ambaye hana haki nchini Kenya. Natarajia kila mwananchi wa Kenya awe na a piece of plot at least na iwe automatic kwa serikali kuhakikisha huyo mtu amepewa kibali cha kupossess that land.

On that note nimeona serikali iko na so much idle resource forest reserves ile kitu inasema eti it is an income generating whatever na mwanachi naye hana chochote. Instead the lions, the baboons are interfering with these na mwanachi hana a piece of plot. The Government should help these people either in the reserves na serikali ikitaka kufanya project irehabilitate these animals in the arid areas using the resources of the donor funds, ndipo mwananchi alime shamba kama hii forest apate chakula kitu cha kwanza.

Kitu kingine land ownership. Tunaelewa kila mtu, hapa tukiwa hivi, out of the a hundred, sixty people hawajapata haki za kumiliki mashamba, because hiyo ministry ina ugumu sana. Tumejaribu. Unapata an indigenous Kenyan tayari ako na title deed lakini mtu ambaye alizaliwa hapa Kenya, ni kizazi cha zamani hana title deed because they way to reach that thing is really complicated. I want to say that there is too much corruption in the land settlement.

Kitu kingine sisi ni wazazi na hatuwezi kusema sisi ndio tunazungumza, mtoto naye nani anazungumza juu yake? Nitaongea juu ya basic needs za watoto kama education. Tunaona ya kwamba mtu yeyote ambaye anajali maslahi ya watoto lazima awe na uwezo wa kuhakikisha every bit of requirement should be easily provided. Tunataka serikali ifikirie jinsi kila mtoto anavyoweza basic education apate. Na ikiwezekana huyo mtoto aelezwe faida za kupata elimu. Zamani tulikuwa tunafikiria unapata elimu ili upate kazi, na sasa kwa vile kazi imekuwa ngumu vile vile tunataka serikali itafute uwezo wa kuhakikisha huyu mtoto atapata elimu na vile vile awajibike kwa sababu amepata elimu.

Kuna vitu vingine kama policies katika education, unasema ya kwamba mtoto asichapwe. Kusema ukweli that is interfering with how somebody brings up a child. Tunaelewa ya kwamba the canning of a child is not killing, unlike I leave my son or my daughter na mwishowe aende awe a victim of these drugs labda ndio hao wanachoma wengine wakiwa shuleni, I don't think that will be proper. Mtoto aadhibiwe kulingana na nafasi yenye anaenda, because there are so many things we should learn from that before you reach the Government. Kwa hivyo the amount of punishment in the school should be spelt out if not, canning to continue.

Political rights, sioni kwa nini civil servants wanakatazwa na wakati unataka kura nitakupigia. How do I elect a president and I am denied that should not practice that? So we want all persons of Kenya to practice politics but to some limits.

Nimeona excessive powers and harassment has been talked about. For sure I don't see how I am a Kenyan and a fellow Kenyan is harassing me starting from the provincial administration, the chiefs and assistant chiefs, those people have powers beyond their knowledge. A junior assistant chief is able to harass a retired police officer, that one I don't think we shall be preserving culture and respect at all at all. I don't see why an assistant chief instead of dealing with petty crime, and domestic issues he can as well advise your woman to go and report you in the law courts, he is promoting what we want to say, a kind of dismantling, he is not actually bringing hao watu together and that is because they are not experienced they are still young. We

want that post to be taken by an elderly person, even if a headmaster has retired he can assume that post because he is experienced, he is elderly, he knows the ethics. Huyo mtoto mchanga atabebeshaje mila ya watu?

Unemployment one man one job; sincerely let us have it that way one man, one job. Kuna watu wako na excessive things. Mtu ako mara hapa, sijui anafanya nini, huko sisi tumekaa tu. Unapata sisi wengine we don't have any job, one man one job.

Interjection Com. Abida Ali: Summarize, malizia.

Francis Wechili: Haya nikimalizia. And we want in job employment tunataka kila community in Kenya ipate nafasi. We have got some jobs huwezi pata makabila fulani, why? The government should look into that. Halafu.....

Interjection Com. Abida Ali: Thank you very much, tutasoma hiyo karatasi.

Francis Wechili: Sitaiwacha kwa sababu it is sketchy.

Interjection Com. Abida Ali: It's okay, we will read it the way it is, don't worry. Thank you. Musavini Gilbert.

Musavini Gilbert: I am Musavini Gilbert. The first one is that our constitution must have a kind of unity. I therefore propose that a constitution should be imposed for over ten years for any alteration to reflect takes place.

Capital punishment which is death penalty, to me it should be removed as a form of punishment since it achieves nothing to the affected instead I propose life imprisonment.

The Member of Parliament performance and responsibility can be increased if a mechanism or a control mechanism is found. I propose that since they owe their allegiance to the constituents a constituency committee be formed to analyze their performance which aims at dismissing or advising the affected; we shall also be able to reduce some of the technical appearance in parliament because we are told that an MP has only to be absent for over or around 8 times. That is so much, at least the constituents should also have a say.

Law is very important, it affects everybody. Therefore for Parliament to transact any business in this country, it needs only 30 members. To me those are very few compared to the number we have of two hundred and twenty two. I therefore propose that a half of members should be able to transact house business.

Nominated MPs to me are now irrelevant because initially they intended to cater for the marginalized, the disadvantaged group. A House of 22 we are able to get the disadvantaged what the initial intention was. So nomination of MPs to me can be done

away with because those who are nominated serve the interests of the nominees.

The role of the Attorney General has to be reduced to enhance efficiency and performance. The AG to me is an MP, he is a minister, and a judge and therefore those offices can be distributed to other people to enhance efficiency and performance.

Finally on(?) that is economic enhancement of each Kenyan is required. Presently we have got people who use money at least to entice others, say Member of Parliament or any other. This is a nutshell promotes corruption because he needs money to give in fund raisings and all these. And therefore I propose that other means should be looked at enabling the local mwananchi to be able to meet his basic requirements. We shall discourage this idea of begging.

Com. Abida Aroni: Thank you, thank you very much. John Olusese, Bi. Kwayero Sasabi.

Kwayero Sasabi: My name is Goyet. Why do we have a President who has lived in this country(?) who will speak something today, tomorrow is changed, that is law. He must be a person who has strength to speak something to people, that things he would do. One day I hear discrimination in this country, that discrimination was said I am going to deal with people from(Inaudible) to Mombasa, but the people from(inaudible) to border of Tanzania to Uganda I will be able to work with them and yet we have brought it to him. Western Nyanza's we have have vote for our leader, why discrimination come?

Second word he himself promised teachers I will do this, therefore after that he has denied saying I will not do. That is not the way to lead. We want a person who has taken the chance of leadership; he must be of reality from diplomatic to upper standards or a graduation who can read everything to know thoroughly without translation.

Interjection Com. Abida Ali: Umemaliza?

Kwayero Sasabi: Not.

Laughter from the audience

Kwayero Sasabi: According to the education opinion we are very very backward. I have reason why, in Europe some years eighteen something Europe was continuously education their people thirty years for science only. Here, we have attempted for this arts and so no job because we have taught one subject and we are unable to promote our children to get employment.

Now we want as Kenyans(?) we try to solve(?) to bring industrial here everywhere near the villages which can help our children to get employment.

Third, I am going to finish with ladies. You ladies of Kenya you are ashaming us very much. Ladies when you have better education you forget your husband and say I am the one I can do whatever I want. How? God wants permanently two people to live together. Am I wrong? No. When you have education you are high you sit there and if your husband is going wrong, be patient and you look after your children.

So, from now otherwise I am going to talk about churches. We have churches who speak very nicely but they don't know how to take care of their people, verbally they never but when you go behind these pastors you get children are there and they cannot have education because there is no payment. This Commission please you will sit and try to help these churches which are very lame to pay their pastors to save children in nursery school please. Thank you.

Com. Abida Ali: Thank you very much ujiandikishe pale Mzee, thank you. Moses Mulunda.

Moses Mulunda: Honorable Commissioners, mimi kwa majina ni Moses L. Mulunda. Jambo la kwanza ambalo ningependa kupendekeza ni kuhusu hizi sheria ambazo zinaonekana zimetupwa wakati wa ukoloni. Ni sheria hii ya kuhusu mwizi na rape. Utakuta kwamba yule ambaye ameiba kuku atafungwa miaka mingi sana kuliko yule ambaye amefanya raping. Sasa ningependelea iwe vice versa yule amefanya raping ambaye amefanya matendo mabaya afungwe miaka mingi na viboko vingi na ule mwingine afungwe miaka kidogo.

Jambo lingine ni kuhusu utamaduni wetu. Utakuta nchi kama Uganda ambapo kulikuwa na wafalme, sasa viongozi waliokuja baadaye wakavuruga na walipouharibu ufalme nchi ikaanza kuendelea vibaya. Hapa pia nchini Kenya tuko na yale makabila yaliyokuwa na ufalme. Ningependekeza kwamba huo ufalme uwe revived.

Jambo lingine ningependa kupendekeza ni kuhusu Kenya Sugar Board. Utakuta tumeambiwa factories kama mbili tatu zimeunganiswa pamoja na utatokea wakati ambapo prices zitakuwa tofauti, ningependekeza kwamba ikiwa kuna factories zile ziliunganishwa pamoja mbili tatu hivi prices ziwe ni zile zile.

Jambo lingine ningependa ni kuhusu civic education. Mtaona ya kwamba kiongozi wa nchi anasema fulani ndiye atanirithi na watu wanalalamika sana na hii inatokea kwa upande wa ukosefu wa civic education, kwa sababu wananchi wanakosa kujua proposing, electing na nominating.

Jambo lingine ni kuhusu hawa wajumbe wa nominated MPs. Wale nominated MPs watoke kwa zile minority tribes kama vile Ogiek, walemavu, wanawake na vijana. Ni hayo tu nilikuwa noyo.

Com. Abida Ali: Thank you, ujiandikishe. Sophia Macy, Jona Liwa.

Jona Liwa: Your honor Commissioners, I am Jona Maliwa from Chiruku location. I would like to say the following:-

Farmers: I would like to appeal to the government at the side of farming it is the most generating project in the country while the input is too high. The price of goods is too low, one remember this year the price of maize is too low, most of the farmers were unable to sell the maize. There- by I propose, the Commissioners at your honor, the price of maize to be increased not less than 1500/=. Most of the majority in Kenya import.

Secondly, employment: mzazi amesomesha mtoto akapita mtihani, ameenda kwa College tena kazi wanasema interview. Interview ya nini na mtoto amepita mtihani? Mambo ya interview watu wanakaa kama mumekaa ndio where tuko na corruption, kama mtoto amepata training, amepita apate kazi immediately. Kutoka mwaka 1998 karibu zaidi ya miaka tano watoto hawajaandikwa. Tafadhali serikali iandike watoto.

Discipline: kila mtu amesoma iko hapa, bila discipline kwa shule watoto hawawezi fanya vizuri. Ukienda Starehe discipline iko high zaidi na shule zingine. Mambo ya discipline vile amesema mtu alikiwa anachapwa zaidi. Bila discipline kwa shule, inategemea na discipline yenyewe unapatia mtoto, bila discipline watoto ndio wanachoma shule na kadhalika. Lazima mtoto apate discipline kulingana na makosa yake, kuliko kuchoma shule aende afungwe, nani anapata hasara? Ni mzazi.

Health, kama hospitali imekuwa kama hali yetu hii Malava district hospital, tafadhali serikali ilete daktari kwa district hospital, ndio daktari mtu akiita daktari anajua mambo yote ugonjwa jinsi anaweza kusaidia wagonjwa. Kwa hayo, finally, asante sana Commissioners.

Com. Abida Ali: Asante jiandikishe tafadhali, jiandikishe pale tafadhali Mzee, asante. Tom Wangusi, Zakayo Indakala.

Zakayo Indakala: Asante sana Commissioners. Mimi naitwa Zakayo Indakala Wemayasi kutoka Kakunga sub location East Kabras. Asanteni sana niko na maneno kidogo ya kuchangisha kwa sababu mengi yamesemwa. Ya kwamba serikali hii ilipokuwepo zamani tulikuwa na price control na watu walikuwa wanaendelea vizuri kuliko sasa kwa sababu mtu anauza kama anavyotaka alafu kuuza kwao kunaleta taabu kwa watu wengine kama akina mama ambao hawana pesa.

Lingine la kwamba mzazi alipata shamba bure kwa mzazi wake, naye ana watoto wake amezaa vijana na amegawanya lakini hajawapa namba, baadaye baba anakufa. Land wanalazimisha yaani sheria inalazimisha ya kwamba wewe ushtaki baba yako ambaye amekufa ndipo ugawie watoto wako shamba au ndipo upate shamba hilo. Watu wanapata hasara ya kuuza mashamba yao ili apate lile shamba pia kwa sababu bei ambayo ya kupata shamba lako ni ghali sana.

Polisi: polisi wa zamani walikuwa na discipline kubwa sana, nzuri sana kwa sababu walikuwa under commissioner pekee yake,

lakini kwa sasa discipline yao iko chini kwa sababu wanasisia wameingilia hawa askari. Ukitaka kumwambia askari amefanya makosa eti mtoto wa fulani ni mkubwa Wanaharass wananchi na hauwezi kusema kwa sababu ni mtoto wa mkubwa.

Utamaduni wa wazee wa zamani: kulikuwa na wazee zamani wanakaa kwa nyumba fulani wanazungumza wakiongea mila za zamani na wanaburudika na busaa kidogo na mrija, si changaa, hiyo walitoa halafu wamefanya serikali inaharass wazee, hata wakipata kama umekaa tu kwa nyumba yako unazungumza na mwenzako unashikwa eti wamefanya makosa unakunywa pombe ilhali unazungunza na mwenzako kwa nyumba. Ningependekeza ya kwamba hao wazee wangepewa uhuru wao wa zamani. Lakini si chang'aa busaa ndio kama zamani kwa sababu kila kabila ilikuwa na mambo ya mila ya watu na iwachiliwe watu wenyewe isiingiliwe.

President awe akifanya kazi kwa miaka kumi kama inayosemekana na watu wengine au na sheria. Asipite miaka ishirini kama iko sasa na awe mtu wa degree.

Chairman wa county council au chairman yeyote ambaye amechaguliwa achaguliwe na wananchi kutoka nyumbani, asichaguliwe na council. Mbunge awe mtu wa degree na councillor awe mtu wa form four. Ni hayo ningependa kuchangisha kwa sababu mengi yamesemwa.

Com. Abida Ali: Thank you. We have Masisai Lotumia, Amos Shamala, Makano Wanami.

Makano Wanami: Commissioners, residents of Malava, I am Makano Wanami. I personally feel the next Government should be a coalition government hence the powers of the president should be reduced hence a President to be non-partisan.

Ten chances should be preserved in Parliament, five for ladies five for youths. Councillors should be of at least O level education and above for proper(Inaudible). Elected leaders who do not perform their duties as per the aspirations and wishes of the electorate they should be eliminated before their term is in office expires..

Education to be free for all Kenyans and medical services also be free. Land title deeds should free for all Kenyans. Provincial administration should be abolished and instead elected leaders should take over their duties. Thank you very much.

Com. Abida Ali: One question, you have said that MPs who do not perform should be eliminated. We should kill them or you mean remove them?

Makano Wanami: I said MPs or elected leaders that is MPs or councilors or President who do not perform their duties as per electorate's aspirations and wishes should be eliminated not to kill.

Com. Abida Ali: What do you mean by elimination?

Makano Wanami: The Electorate should be given an opportunity to remove them from their offices before their terms elapse.

Com. Abida Ali: Okey, thank you, thank you, thank you. Rober Webuye.

Robert Webuye: My name is Robert Webuye. I have a few remarks to make, I mean proposals. Parliament should approve a constitution if well-drafted to accommodate the rights of the public, protect them, the public to exhaust them with justice and the state constitution to remain a block against trespass into justice.

Parliament, when approving this Constitution, to consider land ownership, farming, that is small scale farmer, market for farmers, good administration for good security against rural theft(Inaudible) Now again briefly land ownership, land title deed or certificate identity are acquired through long processes and expensive. It should be short, simple, clear, less taxation and closer to the public.

Farming: small-scale farmers should be uplifted by either through simple loans or the government allocate these farmers a fraction of any foreign aid. In particular it is for early preparation of land, seeds and fertilizers. This is an alternative to reduce poverty and hunger. Market for dairy and crop products should be stabilized to improve the welfare of the farmer.

Administration: the administration is what we need in the rural life, but it is an organ existing in the wrong government since it considers chiefs as KANU prefects. They can even lose their employment in failure to comply with the needs of the party.

Family disputes, land disputes and any disorder with residents in the rural have never been settled with justice. My suggestions are as follows: -

- Reduce the created administration boundaries to avoid idling and incompetence among the chiefs since they are more that their duties and are earning wrong salaries.
- Overhaul the administration if it has to exist, as a cleane organ.
- Clip their powers for concentration of their duties by providing freedom for the public to forward their negligence at the DOs offices.
- However, we should not elect the administration, they are not politicians and they should not behave like politicians.
- Dominant clans will win such elections and will marginalized minority clans.
- They are meant to serve the public without favour.
- At one point there is need to replace the administration by another organized organ but funds to retire all the

administration is a heavy part into the government considering our bad economy.

- Judiciary is very untrustworthy with what we have experienced at the Kakamega law courts, court clerks and magistrates have collaborated in taxing the disputing parties heavily before any verdicts, and the innocent complainants and plaintiffs have been victimized. Provide powers to watch this.
- Political representation: a responsible rural councillor foresight should be above illiterate and this can be reached through strict and right interviews at the nomination of the candidates, or hand written English or hand-written Kiswahili, some bit of Maths, they are enough to clear a candidate and not necessarily a form four but can speak.

Interjection Com. Abida Ali: Malizia sasa, give us your last sentence.

Robert Webuye: The last is Moi day was imposed to Kenyans by the parliament under one party system. Remove this from the constitution as a public holiday since it was not by the demand of the public and it's unnecessary after the Moi regime. Thank you.

Com. Abida Ali: Thank you. Juma Mumasi.

Juma Mumasi: Mimi jina langu naitwa Juma Mumasi, upande wa Kabras P. O. Box 82 Malava. Kusikitika yangu upande wa polisi, unaweza kuwa unatembea na mvua ikupate njiani uingie kwa nyumba ya mtu kujikinga mvua. Hujui kama kuna chang'aa ndani, au ni nini iko ndani. Na polisi wakija wakupate hapo na hata hunywi pombe na hata hujui kama pombe iko ndani ya nyumba. Na polisi atakuja akuweke kwa kamba uende polisi na uende kortini, na hukukula pombe na hata tangu uzaliwe hujawahi onja pombe na hata wewe ni Mkristo. Ukifika kortini unaambiwa kortini ya kwamba unashtakiwa kupatikana na pombe. Ukikataa unaambiwa utakwenda rumande na hiyo sio sheria nzuri. Kwa sababu rumande ni kutisha mtu aitike makosa yale ambayo sio yake. Hiyo sheria itolewe korti kulazimisha mtu kukubali makosa kuharibu sifa yake na yeye sio mkulaji wa pombe.

Ni afadhali korti itake mtawala wake kama sub-chief akuje atoe ushahidi kujua kama huyo mtu anakula pombe, ndio mtu ashtakiwe pale. Hilo neno naona sheria hiyo korti hata ya hatari inalazimisha watu tu ukionyesha mahali kuna makosa polisi hawataki kusikia wanakimbia mahali kuna pombe, gari lao linaenda mahali iko pombe kwa sababu wanajua hiyo sheria ni rahisi utakwenda kubali kortini, sijui kama wanapata madaraka kwa hiyo sheria siwezi kujua. Hiyo sheria ni mbaya, kulazimisha watu kukubali makosa yale ambayo hawayajui. Yeye ni Mkristo anaaminiwa na Ukristo lakini akirudi nyumbani watasema oh naona hao Wakristo wengine

Interjection Com. AbidaAli: Haya uko na jambo lingine Mzee?

Juma Mumasi: Jambo lingine iko.

Interjection Com. AbidaAli: Haya sema.

Juma Mumasi: Jambo la pili, tena bado kortini. Nikishtaki mtu kwa koti na akubali makosa, ngo'mbe yangu alikula na anataka kulipa, korti inakuambia enda urudi tarehe fulani na huyo mtu amekubali. Si kufanya attachment, anarudi ya nini? Kurudi unasikia ati una mshahidi. Hiyo mambo ni mbaya kwa wananchi.

Ya tatu, ng'ombe barabara: unaweza kuwa na ng'ombe unapeleka soko na unaona gari linapelekwa na mtu mwenya macho na ng'ombe inaweza shinda kila mtu hata akuwe minister au rais. Mtu wa gari atagonga ngombe ni lazima ataambiwa ya kwamba ukigonga ng'ombe, gari likigonga ng'ombe uende utengeneze hilo gari kwa sababu ng'ombe imegonga gari na ngombe huwezi kushika. Kwa hivyo hiyo sheria ya barabara na ng'ombe itolewe. Gari lione kama ni ngo'mbe lipunguze mafuta liende kujua ni ngo'mbe kwa sababu ng'ombe inaweza kushinda kila mtu. Mtu hawezi kushinda ng'ombe, ng'ombe ni mnyama. Hiyo sheria itolewe, ng'ombe ichungwe na dereva wa gari kuliko mtu atengeneze gari. Hiyo gari inatengenezwa sasa imeharibika na unamtengenezea ati taa imepasuka itakuwa wewe ukitengeneza.

Com. Abida Ali: Asante. Isaac Malumasi.

Isaac Malumasi: Kwa majina naitwa Isaac Malumasi Box 28 Malava. Ajenda yangu ya kwanza ni hivi, mimi ni jirani wa forest na wakati mipaka ilipita ya forest mwaka wa thelathini na tano wabeberu walikuwa wakija na askari na wanaambia baba zetu ati sasa inatakiwa muondoke kwa haya mashamba yako karibu na forest, serikali inapitisha mipaka kwa forest. Halafu wakafukuza baba zetu na wkapitisha tu mipaka kwa forest ikachukua mashamba yoa ikarudisha kwa forest. Sasa hii mambo ndio sisi tunataka ya kwamba mkienda Nairobi muambie Parliament itengeneze tume ya kuja kuchunguza misitu, ije a round kwa misitu na sisi pia jirani wa misitu tuwe na committee yetu tuwaonyeshe forest yenyewe ilikuwa ikipita hapa hivi na hii mashamba mengine haya walipofukuza baba zetu ndio wakachukua haya mashamba wakarudisha kwa forest. Hili ndilo jambo langu ambalo ninalo.

Jambo lingine la kufuata hilo, tunataka tena watoto wetu kutoka kwa nursery mpaka University wasome bure, na malipo yao sisi wenyewe tutakubali ya kuwa tuna mashamba, kila mtu aliye na heka mia moja awe akitoa kodi kwa kila hekari shilingi ishirini ishirini mpaka hiyo kodi yote iende kwa serikali kusomesha watoto wetu. Hata watu wenye forest tena nao watailipia forest hiyo kodi. Hata wale wanyama wa porini watalipiwa kodi kwa zile hekari zao wanazotumia.

Interjection Com. Abida Ali: Asante Mzee, jiandikishe pale.

Isaac Malumasi: Niende pale?

Com. Abida Ali: Ujandikishe wakati wako umeisha sasa.

Isaac Malumasi: Nina lingine nilikuwa bado sijamaliza.

Com. Abida Ali: Haya la mwisho.

Isaac Malumasi: Ningali nayo mawili. Moja ni kuwa sisi tuna factory yetu hapa ya Western Kenya nayo inatulipisha kwa tani moja ya miwa shilingi 1000/= na factory zote zilizo katika Kenya hulipisha watu, hununa muwa kwa shilingi 2500/=. Kwa hivyo inafaa mpeleke hiyo report Nairobi hawa wajamaa waje watutetee, maana factory hii kwa nini inatuuu zaidi namna hivi na sisi ni wananchi wa Kenya?

La mwisho barabara hii ni nyembamba zaidi. Na kutoka hii barabara huende mpaka Kitale na upande huu huenda mpaka Kisumu mpaka Kisii. Na ukitoka Webuye unakwenda Kitale ni class B barabara na ukitoka Kakamega unakwenda mpaka Kisii ni class B na hapa kwetu Malava ndio walifanya tu class C ikawa nyembamba zaidi. Kwa nini walitudharau namna hivyo? Mpeleke tena kwa parliament watuongeze hii barabara yetu iwe class B ndio sasa iwe pamoja na zingine ndio twende vizuri.

Com. Abida Ali: Asante, sasa jandikishe pale, asante sana. Okey Mukangai Stephen, Chitiari Godwin.

Chitiavi Godwin: Okey thank you, my names are Chitiavi Godwin, I am from around. I would wish to highlight the following :-

